



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli  
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM  
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222  
Faksi: +255 22 2111281  
Barua Pepe: [chragg@chragg.go.tz](mailto:chragg@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

Julai 14, 2015

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

### **Tamko la THBUB kulaani mauaji ya Askari Polisi na raia katika kituo cha Stakishari, Dar es Salaam**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kuuwawa kwa askari polisi wanne na raia watatu, katika tukio linalodaiwa kufanywa na kundi la majambazi waliovamia Kituo cha Polisi cha Stakishari, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam usiku wa tarehe 12 Julai, 2015.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inalaani vikali mauaji haya ya kikatili ya watu wasiokuwa na hatia. Aidha, tunaungana na Watanzania wengine nchini kuwapa pole wafiwa na wote walioguswa na msiba huu.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 14, kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika jamii, kwa mujibu wa sheria. Hivyo, kuuwawa kwa raia, pamoja na askari polisi hawa ambao ni walinzi wa usalama na amani nchini, tena wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kulinda usalama na mali za raia ni kitendo kinachopaswa kulaaniwa vikali na kila mwananchi.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kuvamiwa kwa vituo vya Polisi na kuuwawa kwa askari ni matukio yanayojirudiarudia na yamekuwa yakisababisha hofu miongoni mwa askari, familia zao pamoja na wananchi kwa ujumla.

Hivyo, Tume inaiomba Serikali kuyapa umuhimu wa kipekee matukio haya kwa kufanya uchunguzi wa kina ili kupata majawabu sahihi ili yaweze kudhibitiwa mapema na hivyo kuwahakikishia askari na raia usalama wao.

Aidha, Tume inapenda kuwakumbusha wananchi kuwa vitendo vya ukatili, mauaji, na matendo yote yanayokiuka Sheria yanayofanywa na raia wasio wema ni ukiukwaji wa Sheria na haki za binadamu na misingi ya utawala wa sheria, hivyo Tume inakemea matendo haya na kutaka yapigwe vita.

Tume inaikumbusha Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kuwa jukumu la ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao ni jukumu la msingi, kwa hiyo inashauri kuimarisha ulinzi katika vituo vya polisi ikiwa ni pamoja na kuwapatia vifaa muhimu, na bajeti ya kutosha.

Vilevile Tume inalishauri Jeshi la Polisi kuimarisha doria zake hasa wakati wa usiku, kama ambavyo Tume inavyoona doria zinazofanyika mchana, kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi.

Mwisho, Tume inatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi la Polisi katika kuhakikisha watu waliofanya tukio hili wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo husika ili sheria ichukue mkondo wake.

Imetolewa na:

  
Mhe. Bahame Tom Nyanduga  
**Mwenyekiti**

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Julai 14, 2015